

KENYA PRIMARY SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT

KPSEA 2026

KISWAHILI

602

Mtihani wa Mazoezi

Muda: Saa 1

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Karatasi hii ina maswali 30. Jibu maswali YOTE.
2. Soma mazungumzo, vifungu na maswali kwa makini kabla ya kuchagua jibu.
3. Kila swali lina majibu manne: A, B, C na D. Jibu MOJA pekee ndilo sahihi.
4. Weka majibu yako kwenye karatasi ya kujibia. Usiandike majibu katika karatasi hii.
5. Tumia penseli ya kawaida ya HB kutia kivuli kwenye duara lenye jibu ulilochagua.
6. Tia kivuli katika duara MOJA tu kwa kila swali. Kivuli kisitoke nje ya duara.
7. Andika nambari yako ya mtihani, jina na shule kwenye karatasi ya kujibia. Iweke safi na usiikunje.

JINSI YA KUONYESHA JIBU

Mfano: Chagua neno lifaalo kujaza pengo.

Kalamu ____ iko mezani.

A. hawa B. hili C. hiki D. hii

Jibu sahihi ni D. Tia kivuli katika duara lenye D.

A

B

C

D

Karatasi ya maswali ina kurasa 6. Hakikisha kuwa maswali yote 30 yapo.

Swali la 1 hadi la 5**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Halima: Habari za asubuhi, Omari?

Omari: Nzuri, Halima. Umefika mapema kwenye maonyesho ya kazi za mikono.

Halima: Ndiyo. Nimeleta mkeka niliousuka kwa nyuzi. Naona una kasha lenye picha nzuri.

Omari: Nimelitengeneza kwa vipande vya kadibodi. Nilipanga kuweka penseli ndani yake.

Halima: Samahani, naweza kulishika ili nione namna ulivyounganisha vipande?

Omari: Bila shaka. Lishike hapa chini ili kifuniko kisifunguke.

Halima: Kumbe umetumia gundi kidogo tu! Kwa nini ulipamba sehemu hii kwa duara?

Omari: Duara hizo zinafunika sehemu zilizounganishwa. Pia zinapendeyesha kasha.

Halima: Una ubunifu mzuri. Baada ya maonyesho, unaweza kunionyesha jinsi ya kutengeneza kasha?

Omari: Nitafurahi kukufundisha. Nawe unaweza kunifundisha kusuka mkeka.

Halima: Sawa. Tutabadilishana ujuzi.

1. Jibu lifaalo kwa salamu ya Halima mwanzoni ni lipi?
 - A. Nzuri.
 - B. Marahaba.
 - C. Alamsiki.
 - D. Buriani.
2. Halima anaonyesha adabu anapo
 - A. kufika mapema kwenye maonyesho.
 - B. kutaja mkeka aliouleta.
 - C. kuomba ruhusa kabla ya kushika kasha.
 - D. kuona duara kwenye kasha.
3. Kwa nini Omari anashauri kasha lishikwe chini?
 - A. Ili picha zifutike.
 - B. Ili kifuniko kisifunguke.
 - C. Ili penseli zianguke.
 - D. Ili kadibodi ipinde.
4. Ni jambo gani linaloonyesha kuwa wawili hao wako tayari kushirikiana?
 - A. Wameleta vitu vinavyofanana.
 - B. Wameshindana kupata kasha.
 - C. Wametumia gundi ileile.
 - D. Wamekubaliana kufundishana ujuzi.
5. “Ubunifu” katika mazungumzo haya ni uwezo wa
 - A. kubuni na kutengeneza kitu kwa mawazo mapya.
 - B. kutamka maneno kwa sauti kubwa.
 - C. kuhifadhi vifaa bila kuvitumia.
 - D. kufika mahali kabla ya wengine.

Swali la 6 hadi la 9**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Jioni moja, Sifa alibaki kupanga vifaa vya michezo kwenye Shule ya Tumaini. Aliona kikuku chini ya rafu. Kilikuwa na herufi mbili zilizandikwa upande wa ndani. Hakujua mwenyewe.

Rafiki yake, Kenga, alimshauri akipeleke ofisini. Sifa alifanya hivyo na kumweleza mwalimu mahali alipokipata. Kesho yake, mwalimu alitangaza habari hiyo. Aliwataka waliokipoteza kueleza alama zake bila kukiona. Mwanafunzi mmoja, Rukia, alitaja herufi hizo mbili kwa usahihi. Alisema pia kuwa kilikuwa zawadi ya dada yake.

Mwalimu alimrudishia kikuku. Rukia alimshukuru Sifa. Kenga alitabasamu, akajua ushauri wake ulikuwa na manufaa.

6. Sifa alikiona kikuku alipokuwa
 - A. akipokea zawadi kutoka kwa dada yake.
 - B. akitafta rafiki yake ofisini.
 - C. akipanga vifaa vya michezo.
 - D. akitangaza habari kwa wanafunzi.
7. Mwalimu aliwataka waliodai kikuku wataje alama zake ili
 - A. kila mwanafunzi atengeneze kikuku.
 - B. abaini mwenye kikuku halisi.
 - C. awafundishe kuandika herufi.
 - D. achague mwanafunzi wa kupanga vifaa.
8. Kitendo cha Sifa kupeleka kikuku ofisini kinaonyesha
 - A. uchoyo.
 - B. woga.
 - C. uvivu.
 - D. uaminifu.
9. Neno “manufaa” katika aya ya mwisho lina maana gani?
 - A. Faida.
 - B. Hasara.
 - C. Mashaka.
 - D. Kelele.

Swali la 10 hadi la 12**Soma kifungu na jedwali kisha ujibu maswali.**

Wanachama wa klabu ya mazingira walipanga kukusanya karatasi zilizotumika kwa ajili ya kutengeneza mapambo. Waliziweka sehemu kavu kabla ya kuzitumia. Jedwali linaonyesha idadi ya karatasi zilizokusanywa kwa siku tatu.

Siku	Darasa la 5	Darasa la 6
Jumatatu	18	24
Jumanne	26	19
Jumatano	21	28

10. Ni siku gani darasa la 5 lilikusanya karatasi nyingi zaidi?
 - A. Jumatatu.
 - B. Jumanne.
 - C. Jumatano.
 - D. Siku zote sawa.
11. Kwa nini karatasi ziliwekwa sehemu kavu?
 - A. Ili wanafunzi wasizihesabu.
 - B. Ili rangi yake ibadilike.
 - C. Ili zisiweze kutumiwa tena.
 - D. Ili zisilowe kabla ya kutumiwa.
12. Kulingana na jedwali, kauli gani ni sahihi?
 - A. Darasa la 6 lilikusanya nyingi zaidi kila siku.
 - B. Darasa la 5 lilikusanya chache zaidi Jumanne.
 - C. Darasa la 6 lilikusanya nyingi zaidi kwa siku mbili.
 - D. Madarasa yote yalikusanya idadi sawa Jumatano.

Swali la 13 hadi la 15**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Mgeni anapouliza njia, maelekezo yaliyo wazi humsaidia kufika anakoenda. Mwelekezaji anapaswa kwanza kuhakikisha mahali panapoulizwa. Akikosa kujua njia, ni vyema kusema hivyo na kumwelekeza mgeni kwa mtu anayepajua.

Unapotoa maelekezo, taja alama zinazotambulika kwa urahisi, kama daraja au jengo lenye jina. Eleza hatua kwa mpangilio: mahali pa kuanzia, upande wa kugeukia na mahali pa kusimama. Maneno kama “kulia” na “kushoto” yanapaswa kutumiwa kwa kuzingatia upande ambao msafiri ataelekea. Maelezo mengi yasiyohitajika yanaweza kumchanganya msikilizaji.

Hatimaye, mwombe mgeni arudie maelekezo kwa maneno yake. Hii itakusaidia kubaini kama ameyaelewa. Ukigundua sehemu yenye utata, ifafanue kabla hajaondoka.

13. Mtu asiyejua njia anapaswa kufanya nini?

- A. Kukubali kuwa hajui na kumwelekeza mgeni kwa anayejua.
- B. Kutaja njia yoyote ili ajibu haraka.
- C. Kumwambia mgeni aende upande wa kulia tu.
- D. Kumpa maelezo mengi bila kutaja mahali.

14. Kwa nini mgeni anaombwa kurudia maelekezo?

- A. Ili asafiri bila kutumia alama.
- B. Ili ataje majina ya majengo yote.
- C. Ili mwelekezaji aondoke mapema.
- D. Ili kuhakikisha kuwa ameyaelewa.

15. Neno “utata” katika kifungu lina maana ya

- A. uzuri wa jambo.
- B. hali isiyoeleweka wazi.
- C. utaratibu wa safari.
- D. mwisho wa mazungumzo.

visit www.competencebased.com or call 0710 765 974 for more revision material

Swali la 16 hadi la 20**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 16 hadi****20. Chagua jibu lifaalo zaidi kwa kila nafasi.**

Jana tulitembelea kituo cha kutengeneza vyombo vya udongo. Fundi alituonyesha udongo ____16____ alikuwa ameuchanganya na maji. Tuliona mikono ____17____ ikilainisha udongo huo. Aliunda bakuli ____18____ kuliweka kivulini. Ingawa kazi hiyo ilihitaji subira, fundi ____19____ kufanya kwa uangalifu. Tuliporudi shuleni, kila mmoja ____20____ maelezo kuhusu hatua alizoziona.

16. A. ambao B. ambayo
C. ambalo D. ambazo
17. A. lake B. chake
C. yake D. wake
18. A. wala B. kisha
C. au D. lakini
19. A. tuliendelea B. waliendelea
C. niliendelea D. aliendelea
20. A. aliandika B. waliandika
C. tuliandika D. ziliandika

Swali la 21 hadi la 25**Chagua jibu sahihi.**

21. Chagua wingi wa sentensi: Kikapu hiki kimejaa.

- A. Vikapu hiki vimejaa.
B. Vikapu hivi kimejaa.
C. Vikapu hivi vimejaa.
D. Kikapu hivi vimejaa.

22. Kanusha sentensi: Mlinzi atafungua lango.

- A. Mlinzi hakufungua lango.
B. Mlinzi hatafungua lango.
C. Mlinzi hafungui lango.
D. Mlinzi hajafungua lango.

23. Chagua jibu lenye maana ya kinyume cha neno “karibu”.

- A. Ndani.
B. Chini.
C. Polepole.
D. Mbali.

24. Chagua sentensi iliyo na alama sahihi za kuuliza swali.

- A. Je, utarudi lini?
B. Je utarudi lini.
C. Je, utarudi lini!
D. Je utarudi, lini.

25. Chagua jibu lifaalo: Zawadi aliweka kikombe ____ ya sinia.

- A. kutoka
B. hadi
C. juu
D. kwa

Swali la 26 hadi la 30**Chagua jibu sahihi.**

26. Chagua jibu lifaalo: ____ alichoka, Rehema alimaliza kazi yake.
- A. Kwa sababu
 - B. Ingawa
 - C. Kabla ya
 - D. Ili
27. Chagua sentensi iliyo katika hali ya kutendwa.
- A. Mchezaji alipiga mpira.
 - B. Mchezaji atapiga mpira.
 - C. Mchezaji anapiga mpira.
 - D. Mpira ulipigwa na mchezaji.
28. Kamilisha methali: Mvumilivu hula ____.
- A. mbivu
 - B. mbichi
 - C. chakula
 - D. matunda
29. Kabla ya kuzungumza mbele ya wageni, Juma alipiga moyo konde. Maana yake ni kwamba
- A. alitaka kuondoka.
 - B. alikasirika sana.
 - C. alijipa ujasiri.
 - D. alilala mapema.
30. Chagua jibu lifaalo: Wanafunzi waliketi kimya ____ wakamsikiliza mgeni.
- A. lakini
 - B. kisha
 - C. ingawa
 - D. au

MWISHO WA KARATASI YA MASWALI

2026 KPSEA Kiswahili — Karatasi ya Kujibia

Nambari ya mthani _____

Jina _____

Shule _____

Tia kivuli katika duara MOJA kwa kila swali kwa kutumia penseli ya HB.

- | | | | | | | | | | |
|----|-----|-----|-----|-----|----|-----|-----|-----|-----|
| 1 | (A) | (B) | (C) | (D) | 16 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 2 | (A) | (B) | (C) | (D) | 17 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 3 | (A) | (B) | (C) | (D) | 18 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 4 | (A) | (B) | (C) | (D) | 19 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 5 | (A) | (B) | (C) | (D) | 20 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 6 | (A) | (B) | (C) | (D) | 21 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 7 | (A) | (B) | (C) | (D) | 22 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 8 | (A) | (B) | (C) | (D) | 23 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 9 | (A) | (B) | (C) | (D) | 24 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 10 | (A) | (B) | (C) | (D) | 25 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 11 | (A) | (B) | (C) | (D) | 26 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 12 | (A) | (B) | (C) | (D) | 27 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 13 | (A) | (B) | (C) | (D) | 28 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 14 | (A) | (B) | (C) | (D) | 29 | (A) | (B) | (C) | (D) |
| 15 | (A) | (B) | (C) | (D) | 30 | (A) | (B) | (C) | (D) |